# AMAZING TANZANIA

Toleo Na. 1 | JUNI 2025

Jarida Maalum la Wizaya ya Maliasili na Utalii







## TANZANIA YASHINDA TUZO 27 KATI YA 60 ZA UTALII DUNIANI

TANZANIA Unforgettable!

wizarayamaliasilinautalii

# YALIYOMO


1. Tanzania Yashinda Tuzo 27 Kati ya 60 za Utalii Duniani- **UK. 1**

2. Tanzania Mwenyeji Tuzo za Utalii Duniani kwa Mwaka 2026-**UK. 3**

3. Rais Samia Abainisha Mafanikio Sekta ya Utalii Akihitimisha Bunge la 12 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania- **UK. 5**

4. Bunge Laridhia Marekebisho ya Mpaka wa Hifadhi ya Taifa ya Nyerere-**UK. 6**

5. Raia wa Nchi 71 Kuingia Tanzania Bila Viza- **UK. 8**

6. Waziri Chana Ataka Maboresho ya Kimkakati Sekta ya Nyuki Nchini-**UK. 9**

7. Bilioni 48 Zatengwa Utekelezaji Mkakati wa Wanyama Wakali na Waharibifu-**UK. 10**

8. Maliasili Yatoa Huduma Kidigitali Wiki ya Utumishi wa Umma-**UK. 12**

9. CP. Wakulyamba: Simamieni Majukumu ya Uhifadhi, Msijihusishe na Rishwa-**UK. 14**

10. Tanzania Yashiriki Mkutano wa Kimataifa wa Sera za Utalii Korea Kusini- **UK. 16**


10. Tanzania Yashiriki Mkutano wa Kimataifa wa Sera za Utalii Korea Kusini- **UK. 16**


11. Rais Samia: Serikali Inaendelea Kushughulikia Changamoto ya Uvamizi wa Tembo Simiyu-**UK. 17**

12. Serikali Yahamasisha Wadau Kuwekeza Katika Utalii Endelevu-**UK.18**

13. Serikali Yaanzisha Juhudi Mpya Kuimarisha Sekta ya Utalii-**UK. 20**

14. Serengeti Yaongoza Uhamasishaji wa Utalli Endelevu-**UK. 22**

15. Nyuki Wanogesha Maonesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma-**UK. 23**

16. Tanzania Yapewa Majukumu Shirika la Utalii Duniani-**UK. 24**

17. Serikali Kujenga Ukumbi Mkubwa wa Kimataifa wa Mkutano Arusha- **UK. 26**

18. Waziri Chana Aipongeza Familia ya Chifu Mkwawa-**UK. 27**

19. Tanzania na EU Kushirikiana Sekta ya Maliasili na Utalii-**UK.28**

20. Waziri Chana Awapongeza TAWA kwa Kubuni Mkakati wa Uwekezaji Zanzibar-**UK. 30**

21. Watalii Wataendelea Kulipia kwa Fedha za Kigeni-**UK. 31**

22. Bodi ya Tatu ya Wadhaminiya TaFF Yapongezwa kwa Utendaji Uliotukuka-**UK. 33**

23. Usiyoyajua Kuhusu Chifu Aliyezikwa Katika Kaburi la Mviringo Akiwa Ameketi Mbinga-**UK. 35**

24. Mastaa Wamiminika Tanzania-**UK. 36**



# TANZANIA YASHINDA TUZO 27 KATI YA 60 ZA UTALII DUNIANI

## Na Mwandishi Wetu

Tanzania imeandika historia mpya baada ya kushinda jumla ya Tuzo 27 kati ya Tuzo 60 zilizotolewa kwenye Tuzo za Utalii Duniani (World Travel Awards - WTA), zilizofanyika nchini kwa mara ya kwanza tangu kuanzishwa kwake mwaka 1993.



Katika ushindi huo wa kihistoria, upande wa Serikali umenyakua Tuzo 11 zikiwemo za vivutio bora vya utalii, Bodi bora ya Utalii Afrika, Eneo bora la Utalii Afrika pamoja na Uwanja wa Ndege bora Afrika.

Kwa upande wa sekta binafsi, kampuni mbalimbali za utalii, hoteli na huduma za kitalii zimefanikiwa kutwaa Tuzo 16. Hizi ni pamoja na Kampuni bora za Utalii wa Safari, hoteli zenye huduma bora, pamoja na hoteli zenye fukwe bora zinazovutia watalii kutoka kona zote za dunia.





Mafanikio hayo makubwa yamechangiwa kwa kiasi kikubwa na juhudi za Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, kupitia hatua mbalimbali ikiwemo uzinduzi wa filamu ya Royal Tour iliyotangaza vivutio vya nchi kimataifa, kuongeza bajeti ya sekta ya utalii, kuboresha miundombinu kwenye maeneo ya hifadhi na kuweka mazingira rafiki kwa wawekezaji.

Ushindi huo umeonesha wazi Tanzania imejipambanua kama kitovu cha utalii barani Afrika na duniani, ikiwa na dhamira ya kuendeleza utalii endelevu utakaowanufaisha wananchi na kukuza pato la taifa.

Hafla ya Utoaji Tuzo za Utalii Duniani ilifanyika kwenye Hoteli ya Johari Rotana jijini Dar es salaam tarehe 28.06.2025.












# TANZANIA MWENYEJI TUZO ZA UTALII DUNIANI KWA MWAKA 2026

**Na Mwandishi Wetu**

Baada ya kuandaa kwa mafanikio makubwa Tuzo za Utalii za Dunia (World Travel Awards) Kanda ya Afrika na Bahari ya Hindi , Tanzania imepata heshima ya kuwa mwenyeji wa hafla ya utoaji wa tuzo hizo ngazi ya dunia mwaka 2026.

Uamuzi huo umetangazwa rasmi na Rais wa Tuzo hizo, Graham Cooke kwenye hafla ya 32 ya Utoaji Tuzo za Utalii Duniani zilizofanyika Johari Rotana jijini Dar es salaam tarehe 28.06.2025.

Akitoa Tangazo hilo Graham amepongeza juhudi kubwa zilizofanywa na Serikali ya Tanzania katika kukuza sekta ya utalii nchini.

Hafla ya Utoaji Tuzo za Utalii kwa Kanda ya Afrika na Bahari ya Hindi imeacha alama kubwa ya kitaifa na kimataifa, ambapo Tanzania ilionyesha uwezo wa hali ya juu katika maandalizi, mapokezi na ugeni, ukarimu na ubunifu.





Graham Cooke ameeleza kuwa mazingira mazuri, ukarimu wa Watanzania, na uwepo wa vivutio vya kipekee vya utalii vimeifanya Tanzania kuwa chaguo bora kwa tukio la ngazi ya juu kabisa duniani katika sekta ya utalii.

Tukio la mwaka 2026 linatarajiwa kuvutia wadau wa utalii kutoka mataifa mengi zaidi na kuchochea ukuaji wa sekta hiyo nchini.





# RAIS SAMIA ABAINISHA MAFANIKIO SEKTA YA UTALII AKIHITIMISHA BUNGE LA 12 LA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**Na Mwandishi Wetu**

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe.Dkt Samia Suluhu Hassan akihutubia na kuhitimisha shughuli za Bunge la 12 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 27.06.2025 amebainisha mafanikio sekta ya Maliasili na Utalii ambapo amesema Serikali ya awamu ya sita imechukua hatua mahususi kuhakikisha sekta ya utalii inaendelea kukua zaidi na kuongeza mchango wake katika pato la Taifa

Hatua mbalimbali zilizochukuliwa na Serikali zimechangia ongezeko la idadi ya watalii wa Kimataifa kwa asilimia 132.1% kutoka watalii 922,692 kwa mwaka 2021 hadi watalii 2,141,895 mwaka 2024.

Vile vile, Rais Dkt.Samia amebainisha ongezeko kubwa la watalii wa ndani kutoka watalii 788,933 mwaka 2021 hadi watalii millioni 3,218,552 mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia 307.9%.

Aidha, Rais Samia ameongeza kuwa maboresho yaliyofanywa kwenye sekta ya utalii yamechochea ongezeko la ajira kwa vijana wa kitanzania kupitia sekta ya utalii ambapo idadi ya wakala za Biashara za utalii zimeongezeka kutoka 2,885 mwaka 2020 hadi kufikia 3,735 mwaka 2025.

"Idadi ya waongoza watalii imeongezeka kutoka waongoza watalii 5,076 mwaka 2020 hadi kufikia idadi ya waongoza watalii 7,662 mwaka 2025"

Pia, mapato yatokanayo na utalii yamepanda kutoka dola za kimarekani millioni 700 mwana 2020 hadi kufikia billioni 3.9 mwaka 2024.





# BUNGE LARIDHIA MAREKEBISHO YA MPAKA WA HIFADHI YA TAIFA NYERERE

**Na Mwandishi Wetu**

Bunge limeridhia ombi la Serikali la kumega sehemu ya Hifadhi ya Taifa ya Nyerere kwa lengo la kutatua migogoro ya mipaka na kuwezesha shughuli za maendeleo kuendelea katika mazingira rafiki kwa jamii na uhifadhi.

Waziri wa Maliasili na Utalii, Mhe. Balozi Dkt. Pindi Hazara Chana, akiwasilisha azimio hilo bungeni tarehe 26.06.2025, amesema Serikali imeamua kumega eneo lenye ukubwa wa kilomita za mraba 1,617 kutoka Hifadhi ya Taifa ya Nyerere na kuwarejeshea wananchi,Pori la Akiba Selous na kwa ajili ya shughuli nyingine za maendeleo

Amesema hatua hiyo imepunguza ukubwa wa hifadhi hiyo kutoka kilomita za mraba 30,893 hadi kufikia kilomita za mraba 29,276.

Akifafanua zaidi, Mhe. Chana amesema hatua hiyo inalenga kuondoa migogoro ya muda mrefu ya mipaka baina ya hifadhi hiyo, vijiji vinavyoizunguka, Pori la Akiba Selous na Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori za Mbarang'andu, Juhiwangumwa, Iluma, Jukumu, Magingo na Nalika.



"Kwa kufanya hivyo, tunaimarisha usalama wa maeneo yaliyohifadhiwa, tunajenga mahusiano bora kati ya wananchi na hifadhi, na kuondoa migogoro iliyodumu kwa muda mrefu," amesema Mhe. Chana.




"Kwa kufanya hivyo, tunaimarisha usalama wa maeneo yaliyohifadhiwa, tunajenga mahusiano bora kati ya wananchi na hifadhi, na kuondoa migogoro iliyodumu kwa muda mrefu," amesema Mhe. Chana.

Aidha, Waziri Chana ameeleza kuwa marekebisho hayo ya mpaka yanalenga kulinda mfumo ikolojia muhimu unaounganisha Hifadhi ya Taifa ya Nyerere na Pori la Akiba Selous, sambamba na kuhakikisha mtiririko endelevu wa maji katika Mto Rufiji, ambao ni chanzo kikuu cha uzalishaji umeme kupitia Mradi wa Bwawa la Mwalimu Julius Nyerere (JNHPP).

Mhe. Chana amebainisha kuwa hatua hiyo itaongeza tija kwa Taifa kwa kuimarisha shughuli za utalii, uwindaji wa kitalii katika Pori la Akiba Selous na maeneo yanayozunguka, na hivyo kuchangia mapato ya ndani kupitia sekta ya utalii.

"Kwa sasa, tunaelekea katika uboreshaji wa uhifadhi wa maliasili kwa ujumla wake – wanyamapori, mimea, mazalia ya viumbe wa majini na pia kuongeza upatikanaji wa maji kwa matumizi ya wakulima, wafugaji na wavuvi," ameongeza.





# RAIA WA NCHI 71 KUINGIA TANZANIA BILA VIZA

**Na Mwandishi Wetu**

Serikali imeingia makubaliano na nchi mbalimbali ili kurahisisha utaratibu wa viza ambapo raia wa nchi 71 hawahitaji viza wanapoingia nchini.

kwa sasa watalii kutoka mataifa mengi zaidi duniani wanaruhusiwa kupata visa wanapowasili (visa on arrival) kwenye viwanja vya ndege vya kimataifa kama Julius Nyerere (Dar es Salaam), Kilimanjaro na Zanzibar.

Haya yamebainishwa na Naibu Waziri wa maliasili na utalii Mhe. Dunstan Kitandula(Mb) alipokuwa akijibu swali la Mhe. Dkt. Pius Stephen Chaya aliyetaka kujua ni jitihada gani zimefanyika kurahisisha upatikanaji wa VISA kwa Watalii wenye uraia tofauti wanaokuja nchini kwa mwitikio wa Tanzania the Royal Tour.

Aidha Mhe. Kitandula aliongeza kuwa Serikali imeendelea kuboresha utaratibu wa utoaji wa viza nchini ili kuendana na mabadiliko ya teknolojia duniani. Mathalan, Serikali kupitia Idara ya Uhamiaji imeanzisha mfumo wa maombi ya viza kwa njia ya mtandao (e-Visa) unaowawezesha watalii kuomba viza popote walipo duniani bila kulazimika kufika ubalozini.

"Halikadhalika, Serikali imeboresha Kanuni za Uhamiaji za mwaka 2023 (GN 428) ambapo kwa sasa watalii wanaotumia Visitors Pass wanaruhusiwa kutembelea Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki na kurejea Tanzania bila hitaji la kuomba upya pasi ya kuingia nchini" Alisema Mhe. Kitandula

Suala la visa lina uhusiano wa moja kwa moja na sekta ya utalii, Wizara ya Maliasili na Utalii imeimarisha ushirikiano na Wizara ya Mambo ya Ndani, hususan Idara ya Uhamiaji, katika nyanja mbalimbali ikiwemo ukusanyaji wa takwimu za watalii na kuwa na mikakati ya pamoja ya kuvutia watalii na fursa za uwekezaji.

Aidha, siku za hivi karibuni, Wizara kupitia Chuo cha Taifa cha Utalii imetoa mafunzo ya Huduma kwa Wateja na Ukarimu kwa Maafisa wa Jeshi la Uhamiaji ili kuboresha huduma zinazotolewa kwa wageni wanaoingia nchini, ikiwemo watalii.



# WAZIRI CHANA ATAKA MABORESHO YA KIMKAKATI SEKTA YA NYUKI NCHINI

**Na Mwandishi Wetu**

Waziri wa Maliasili na Utalii, Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana (Mb) ameelekeza kujengwa kwa maabara za kupima ubora wa asali nchi nzima sambamba na kufanya tathmini muundo wa kada ya ufugaji nyuki kwa lengo la kuikuza Sekta ya Ufugaji Nyuki.

Ameyasema hayo katika kikao cha 17 cha kamati ya Taifa ya Ushauri ya Maendeleo ya ufugaji nyuki (NABAC) kilichofanyika Juni 23, 2025 katika ukumbi wa mikutano wa Chuo cha Taifa cha Utalii jijini, Dar es salaam

“Tayari tuna maabara ya mazao ya nyuki iliyopo Njiro, hizi maabara tunahitaji nyingi za kutosha ili zihudumie Tanzania nzima hivyo tuangalie namna gani kila mkoa uwe na maabara” amesisitiza Mhe. Chana.

Aidha amesema wakati umefika wa kuangalia kwa ukaribu kada ya ufugaji kuona ya kuboresha mshahara na maslahi mengine na kuhakikisha kunakuwa na vikao vya mara kwa mara kusikiliza changamoto zao na mawazo ya kuikuza sekta hiyo.

“Naelekeza tuwe na kikao cha maafisa nyuki Tanzania nzima kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI tupate mawazo yao kwa sababu ajira zao zimekuwa changamoto” amesema Mhe. Chana.

Aidha,Mhe. Chana ameipongeza kamati hiyo kwa mafanikio iliyoyapata katika Wizara ya Maliasili na Utalii baada ya kumaliza muda wake wa kuhudumu kwa mujibu wa sharia kwa kipindi cha miaka mitatu.

Naye, Mwenyekiti wa Kamati ya NABAC, Bw. Jackson Msome amesema kamati hiyo imepata mafanikio mengi na kati ya hayo ni pamoja na Tanzania kupata nembo ya asali itakayotumika kuitangaza asali katika soko la ndani na nje ya nchi pamoja na kutolewa kwa msahama wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwenye baadhi ya vifaa muhimu kwenye uchakataji wa mazao ya nyuki.



# BILIONI 48 ZATENGWA UTEKELEZAJI MKAKATI WA WANYAMA WAKALI NA WAHARIBIFU

**Na Mwandishi Wetu**

Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2025/2026, imetenga jumla ya Shilingi bilioni 48.3 kwa ajili ya kutekeleza mkakati wa kukabiliana na changamoto ya wanyamapori wakali na waharibifu ambao wamekuwa wakiathiri maisha na mali za wananchi katika maeneo mbalimbali nchini.

Haya yamesemwa na Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mhe. Dunstan Kitandula alipokuwa akichangia Bajeti kuu ya Serikali kuhusu Wizara ya Maliasili na Utalii bungeni jijini Dodoma.

Amesema Wizara itatekeleza kazi mbalimbali ikiwa ni pamoja na ununuzi wa helikopta 2, ndege nyuki (drones) 12, mikanda maalum ya mawasiliano (GPS Satellite Collars) 50, na mabomu baridi 40,000 kwa ajili ya kufuatilia na kuzuia uvamizi wa wanyamapori.



Vilevile, mabwawa 12 na visima vya maji 18 vitachimbwa katika maeneo mbalimbali ya hifadhi, kujenga uzio wa umeme wenye jumla ya urefu wa kilometa 53 na vituo 19 vya askari katika maeneo yenye changamoto kubwa.



"Katika hatua nyingine, Wizara itajenga vizimba 50 katika maeneo yanayokumbwa na changamoto ya mamba na viboko kwa ajili ya kuongeza usalama kwa wananchi pamoja na kutoa mafunzo kwa Askari Wanyamapori wa Vijiji (VGS) 100 ili kuongeza uwezo wa jamii kushiriki kikamilifu katika juhudi za kukabiliana na changamoto hizi" Alisema

Aidha, Mhe. Kitandula alisema hadi kufikia Aprili 2025, jumla ya tani 1,321.35 za asali zenye thamani ya shilingi 15,856,164,000.00 zimeuzwa nje ya nchi sawa na asilimia 206.9 ikilinganishwa na kiasi cha tani 430.61 zenye thamani ya Shilingi 5,167,332,000.00 zilizouzwa nje ya nchi kwa kipindi kama hicho mwaka 2024.

Kwa maendeleo haya, Shirika la Wafugaji Nyuki Duniani limeiteua Tanzania kuwa mwenyeji wa Mkutano wa Wafugaji nyuki duniani (APIMONDIA) mwaka 2027, utakaohudhuriwa na watu zaidi ya 4,000 kutoka sehemu mbalimbali za dunia.




# MALIASILI YATOA HUDUMA KIDIJITALI WIKI YA UTUMISHI WA UMMA

**Na Mwandishi Wetu**

Wizara ya Maliasili na Utalii kupitia Idara na Taasisi zake mwaka 2025 ilijipanga kuwahudumia wananchi kwa njia ya kidijitali katika maonesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma yaliyofanyika katika viwanja vya Chinangali Park, jijini Dodoma.

Akizungumza kuhusu ushiriki wa Wizara hiyo, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dkt. Hassan Abbasi amesema kuwa huduma nyingi zinazotolewa kwenye banda la Wizara hiyo zinaendeshwa kwa mfumo wa kidijitali, hatua inayolenga kuongeza ufanisi, uwazi na uwajibikaji.

"Idara na Taasisi zetu zimejiandaa vyema kutoa huduma kwa njia ya teknolojia, wananchi wanapata taarifa nyingi kupitia simu zao janja kwa kutumia QR Code, kuhusu uhifadhi, utalii na fursa mbalimbali zilizopo katika sekta hii muhimu," amesema Dkt. Abbasi.



Ameeleza kuwa mkakati wa kuimarisha huduma za kidijitali ni sehemu ya kujibu mahitaji ya watalii wa kisasa na matokeo ya juhudi za Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kupitia filamu za 'The Royal Tour' na 'Amazing Tanzania', ambazo zimeitangaza Tanzania kimataifa.

Mbali na huduma hizo, wananchi pia walipewa elimu ya Tiba Nyuki, taarifa za utafiti kuhusu wanyamapori na misitu, pamoja na fursa za kiuchumi kwenye sekta za malikale, misitu, nyuki, na wanyamapori.

Maonesho hayo yalianza Juni 16- 23, 2025, yakiwa na kaulimbiu: "Himiza Matumizi ya Mifumo ya Kidijiti ili Kuongeza Upatikanaji wa Taarifa na Kuchagiza Uwajibikaji."



# CP. WAKULYAMBA:SIMAMIENI MAJUKUMU YA UHIFADHI, MSIJIHUSISHE NA RUSHWA

**Na Mwandishi Wetu**

Maofisa na Askari wapya wa Jeshi la Uhifadhi wa Mamlaka ya Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) wametakiwa kusimamia ipasavyo majukumu ya uhifadhi katika maeneo watakayopangiwa ili kuimarisha ulinzi wa rasilimali za taifa na kujiepusha na vitendo vya rushwa.




Wito huo umetolewa na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Kamishna wa Polisi Benedict Wakulyamba alipokuwa akifunga mafunzo ya Maofisa na Askari hao 238 katika Kituo cha Mafunzo Mlele, mkoani Katavi.

CP. Wakulyamba amesisitiza kuwa hatua hiyo ni sehemu ya kuunga mkono juhudi za Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, katika kulinda mazingira na rasilimali za taifa na kuwasihi kujenga mshikamano, nidhamu na maadili mema katika utendaji wao wa kazi.

"Hakikisheni mnakuwa waadilifu, watiifu na wanyenyekevu katika utekelezaji wa amri halali kutoka kwa viongozi wenu na kamwe msijihusishe na vitendo vya rushwa,"amesema.





Ameongeza kuwa "Jeshi la Uhifadhi halitavumilia askari au Ofisa yeyote atakayehujumu juhudi za uhifadhi kwa kupokea rushwa au kuruhusu shughuli haramu kama uingizaji wa mifugo na uchimbaji wa madini ndani ya hifadhi."

Naibu Katibu Mkuu huyo amewapongeza Askari na Maofisa wote waliomaliza mafunzo hayo kwa mafanikio na kuwashukuru wakufunzi waliojitolea kuhakikisha mafunzo ya miezi sita yanafanikishwa kwa ubora unaotakiwa.

Mafunzo hayo ni sehemu ya maboresho ya utendaji katika Jeshi la Uhifadhi la TANAPA na wahitimu 238 waliohitimu kati yao, 229 ni Askari waliopitia kozi ya awali ya Jeshi la Uhifadhi, watatu wamehitimu kozi ya mabadiliko ya muundo wa utendaji kazi na sita wamehitimu kozi ya Uongozi kwa Askari Uhifadhi waliopandishwa vyeo kuwa maofisa.






# TANZANIA YASHIRIKI MKUTANO WA KIMATAIFA WA SERA ZA UTALII KOREA KUSINI

**Na Mwandishi Wetu**

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii anayeshughulikia masuala ya Utalii, Mabula Nkoba ameongoza ujumbe wa Tanzania kushiriki katika Mkutano wa Ngazi ya Juu wa Sera za Utalii – 2025 (KOPIST High-Level Tourism Policy Forum) unaofanyika Korea Kusini.

Mkutano huo umeandaliwa na Wizara ya Michezo, Utamaduni na Utalii ya Korea Kusini kwa kushirikiana na Shirika la Utalii la Korea (KTO), kupitia mpango wa ushirikiano wa KOPIST unaolenga kuendeleza utalii endelevu.

Katika mkutano huo, Tanzania ni miongoni mwa nchi 11 kutoka mabara mbalimbali zinazoshiriki mkutano huo kwa lengo la kuimarisha ushirikiano katika sekta ya utalii wa ikolojia na utalii unaozingatia jamii.

Katika hotuba yake, Nkoba ameeleza kuwa Tanzania imejaliwa vivutio vya kipekee kama Mlima Kilimanjaro, Hifadhi ya Serengeti, Ngorongoro, Ruaha na visiwa vya Zanzibar, ambavyo vinachangia zaidi ya asilimia 17 ya Pato la Taifa (GDP).

Amesisitiza umuhimu wa kushirikisha jamii katika shughuli za utalii na kutoa wito kwa wawekezaji kutoka Korea Kusini kushirikiana na Tanzania katika kuimarisha miundombinu, huduma rafiki kwa mazingira na bidhaa mpya za utalii kama MICE na utalii wa picha.

Ujumbe wa Tanzania umeambatana na maofisa kutoka TAWA na TANAPA, ambao pia wanapata fursa ya kujifunza mbinu za kisasa za kukuza utalii wa kidijitali na wa makundi maalum.




# RAIS SAMIA: SERIKALI INAENDELEA KUSHUGHULIKIA CHANGAMOTO YA UVAMIZI WA TEMBO SIMIYU

**Na Mwandishi Wetu**

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amesema Serikali inaendelea kuchukua hatua madhubuti kutatua changamoto ya uvamizi wa tembo katika Wilaya ya Meatu, mkoani Simiyu, ambao wamekuwa wakiwasumbua wananchi na kuhatarisha maisha na mali zao.

Akihutubia wananchi wa Meatu Juni 17, 2025 wakati wa Ziara yake mkoani Simiyu amesema tayari Serikali imejenga vituo vitatu vya askari wa uhifadhi kama sehemu ya juhudi za kudhibiti wanyamapori hao wakali.

Aidha, amemtaka Mbunge wa Kisesa, Mhe. Luhaga Mpina, kuendelea kufuatilia kwa karibu suala hilo kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii endapo hali itaendelea kuwa tete.

"Kuhusu uvamizi wa tembo, mambo haya yanafanyika hatua kwa hatua. Kama tumeweza kujenga vituo vitatu vya askari uhifadhi, basi ni wazi kuwa tutaendelea kuchukua hatua zaidi. Lakini kama tatizo litakuwa kubwa, basi umuone Waziri wa Maliasili na Utalii," amesema Rais Samia.

Katika hatua nyingine, Rais Samia amezungumzia maendeleo ya sekta ya utalii katika mkoa huo na kusema kuwa ukamilika kwa ujenzi wa daraja la Itembe kutakuwa kichocheo kikubwa cha kukuza utalii wilayani Meatu.

"Daraja hilo litawawezesha watalii kufika kwa urahisi katika hifadhi za Maswa, Ngorongoro na Serengeti kupitia Meatu, hivyo wananchi wanapaswa kujipanga vizuri kunufaika na fursa hiyo.

Awali, Mbunge Mpina ameiomba Serikali kuongeza bajeti na rasilimali zaidi kwa ajili ya kudhibiti wanyamapori wakali, hasa tembo, ambao wamekuwa wakiharibu mazao na makazi ya wananchi.






# SERIKALI YAHAMASISHA WADAU KUWEKEZA KATIKA UTALII ENDELEVU

**Na Mwandishi Wetu**

Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira Mhe. Khamis Hamza Khamis ametoa wito kwa wadau katika sekta ya utalii kuongeza uwekezaji na juhudi za pamoja katika usimamizi wa utalii katika maeneo yanayolindwa ili kuwa na Utalii endelevu.

Mhe. Khamis ameongeza kuwa kuwekeza katika utalii wa maeneo yaliyolindwa sio tu kunafaida kwa uhifadhi, bali pia unahamasisha maendeleo ya kimkakati ya jamii inayozunguka maeneo hayo.

Akifunga warsha ya kujadili umuhimu wa Uhifadhi, Ukuaji wa Utalii na Ustawi wa Jamii iliyofanyika kwenye hotel ya Mt. Meru jijini Arusha Juni14,2025 amesema ni wakati sasa wadau kujitokeza kwa wingi kuwekeza na kujikita katika usimamizi wa Rasilimali za utalii ili ziweze kutuletea faida kwa jamii na Taifa kwa ujumla.

Pia amesisitiza juu ya umuhimu wa kubadilishana uzoefu utakaosaidia katika kuchunguza fursa zilizopo kwenye Maliasili zitakazoweza kunufaisha jamii kama kichocheo muhimu cha maendeleo.

Amesema bila wanayama hakuna Utalii, bila misitu hakuna utalii hivyo ni vyema tukahamasisha watu kutumia nishati safi ili kuendelea kutunza misitu yetu, kulinda na kuhifadhi wanyama wetu ili utalii uendelee na uingize pato kwa Taifa na jamii ya maeneo husika ipate manufaa.

Akizungumza wakati wa warsha huyo ya Mkurugenzi wa Benki ya Dunia Kanda ya Tanzania Nathan Belete amesema kukuza ushirikiano kati ya wadau ni njia bora ya kusaidia juhudi za uhifadhi.



"Utafiti umeonesha kuwa utalii katika maeneo yanayolindwa una faida kubwa, unatoa ajira, na unaingiza Taifa pato kubwa ambalo hurudishwa kwa jamii kwa kuwekezwa katika miradi ya maendeleo'

Alibainisha kuwa, katika baadhi ya nchi, kila dola moja iliyowekezwa katika maeneo yanayolindwa huzalisha hadi dola 28 ambapo ni faidi kwa jamii na Taifa kwa ujumla.



# SERIKALI YAANZISHA JUHUDI MPYA KUIMARISHA SEKTA YA UTALII

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imeanza hatua ya kimkakati kuhakikisha tunakua na Utalii endelevu kwa kuzingatia mabadiliko yanayoendelea kutoka kuwa nchi ya kipato cha chini hadi nchi ya kipato cha kati cha juu.

Mkakati huu unaenda sambamba na mikakati ya awali na hatua mbalimbali zilizoanza kutekelezwa zinazokusudia kuendeleza sekta ya utalii, kusaidia uhifadhi na maisha ya watu kupitia uhifadhi na utalii.

Akizungumza katika warsha ya kujadili kuhusu Uhifadhi na Mchango wake katika Utalii na Maendeleo ya Jamii Tanzania', Waziri wa Maliasili na Utalii, Balozi Dkt. Pindi Chana amesema Tanzania inapotoka katika nchi ya kipato cha chini hadi kipato cha kati mabadiliko makubwa yanatarajiwa na kama nchi hatutikiwi kuendelea kutegemea fedha za misaada na ruzuku pekee bali kuwa mshirika wa kimkakati katika maendeleo.

Dkt. Chana amesema lazima tuhakikishe tunakua na Utalii endelevu utakaomnufaisha kila mmoja wetu , licha ya mafanikio yaliyopatikana kwa upande wa wageni na mapato, juhudi zaidi zinahitajika ili kuweza kuongezeka maradufu kwa idadi na wageni na mapato yetu kwa ujumla na kuhakikisha pia jamii inanufaika.



Nchi yetu inaongoza kwa kuwa na idadi kubwa ya simba, chui, nyati na tunashika nafasi ya 3 duniani kwa kuwa wengi na Tembo, tuna tamaduni na ukarimu wa kuvutia; fukwe bora na viumbe wa baharini; maziwa mengi ambayo yanaweza kutumika kuimarisha utalii na kusaidia sekta nyingine za maendeleo,"

Dkt. Chana ameitaka Wizara kuendeleza Tafiti katika sekta ya utalii ambao utaliwezesha Taifa kuwa katika nafasi nzuri ya ya kunufaika na Utalii huku ikiendelea kuhifadhi rasilimali zake.



Tusiridhike na mafanikio tuliyopata kama ongezeko la wageni kutoka milioni 1.7 mwaka 2021 hadi milioni 5.3 mwaka 2024 na mapato ya utalii kuongezeka kutoka bilioni 1.3 hadi Dola za Kimarekani bilioni 3.9 ila tuongeze jitihada tupate mafanikio zaidi ya haya.

Warsha hii imeandaliwa na Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Ushirikiano na Benki ya Dunia nanunafanyika katika jiji la Arusha kuanzia tarehe 13 - 14 Juni, 2025 ukiwa na lengo la kuangazia namna Tanzania inavyoweza kuboresha maendeleo ya sekta ya utalii, kusaidia uhifadhi na kuboresha maisha ya watu wkupitia uhifadhi na utalii.

Warsha hiii ni sehemu ya juhudi za Serikali katika kuendeleza na kutekeleza mikakati ambayo inaimarisha utengenezaji wa mapato ndani ya maeneo yaliyohifadhiwa.



# SERENGETI YAONGOZA UHAMASISHAJI WA UTALII ENDELEVU



**Na Mwandishi Wetu**

Jukwaa kubwa la Kimataifa la "NewsBytes" limeitaja Hifadhi ya Taifa Serengeti kuwa kinara wa uhamasishaji wa utalii endelevu barani Afrika

Kupitia makala ya " Five Wildlife Sanctuaries Promoting Sustainable Tourism" iliyochapishwa Juni 12, 2025 imeitaja Serengeti kuwa kinara katika juhudi zake za kulinda mazingira, kuhifadhi bioanuwai na kushirikisha jamii katika shughuli za uhifadhi na utalii kwa ajili ya maendeleo endelevu ya sekta ya utalii nchini.

Mbali na Serengeti, "NewsBytes" pia imezitaja hifadhi nyingine bora kwa utalii endelevu barani Afrika kama vile Kruger (Afrika Kusini), Maasai Mara (Kenya), Bwingi (Uganda) na Etosha (Namibia) ambapo hifadhi hizo zinajulikana kwa juhudi za uhifadhi, utalii endelevu na ushirikishwaji wa jamii.

Kutajwa kwa Hifadhi ya Taifa Serengeti ni ishara kuwa Tanzania inaendelea kuwa kinara katika uhifadhi wa kisasa unaojali mazingira na jamii.

Vivutio kama uhamaji wa Nyumbu (The Great Wildebeest Migration), wanyama wakubwa watano maarufu kama "The Big Five" na mandhari ya kuvutia vinaifanya Serengeti kuendelea kuzishinda hifadhi nyingi barani Afrika na dunia kwa ujumla.






# NYUKI WANOGESHA MAONESHO YA WIKI YA UTUMISHI WA UMMA

**Na Mwandishi Wetu**

Wananchi wengi wameendelea kumiminika katika Banda la Wizara ya Maliasili na Utalii lililopo kwenye maonesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma Jijini Dodoma kujipatia huduma muhimu zinazohusu Idara na Taasisi zake hasa tiba ya kung'atwa na Nyuki.

Akizungumzia mwenendo wa wageni kwenye Banda hilo, Mratibu wa maonesho hayo kwa Banda la Wizara ya Maliasili na Utalii, Bw. Alexander Mwita, amesema licha ya wageni wengi kupatiwa hudama na wataalam wa Idara na Taasisi zingine lakini wengi wamejitokeza kupata huduma ya tiba hiyo ambayo ni nadra sana kutolewa.

Ameongeza kuwa tangu maonesho hayo yaanze ameshuhudia watu wakirudia zaidi ya mara mbili kwenye banda hilo kudungwa na mdudu nyuki ili kuimarisha kinga dhidi ya magonjwa mwilini.

"Tunaendelea kuwakaribisha wananchi wote, waje tuwahudumie, utakapofika hapa utakutana na Idara na Taasisi za Wizara yetu, hii inawarahisishia kupata huduma mahala pamoja ukilinganisha na kufuata huduma huko zilipo. Wakifika hapa hawatajutia". Alisema Bw. Mwita.

Naye Bw. Aloyce Ezekiel mkazi wa Ilazo Jijini Dodoma licha ya kupongeza jitihada za Wizara hiyo za kuwafikishia hudama kwenye maonesho hayo, ameshauri elima ya tiba nyuki itolewe mashuleni ili kuwarithisha watoto Utamaduni wa kumthamini mdudu huyo mwenye mchango mkubwa kwa uchumi nchini.

Maonesho hayo yaliyobeba kaulimbiu "Himiza Matumizi ya Mifumo ya Kidijitali ili kuongeza Upatikanaji wa Taarifa na Kuchagiza Uwajibikaji" yalifunguliwa rasmi tarehe 16 Juni 2025 na yanatarajiwa kufungwa rasmi tarehe 23 Juni 2025, Jijini Dodoma.




# TANZANIA YAPEWA MAJUKUMU SHIRIKA LA UTALII DUNIANI

**Na Mwandishi Wetu**

Tanzania imechaguliwa kuwa mjumbe wa Kamati ya Hati za Uwakilishi katika Shirika la Utalii Duniani, kamati ambayo hushughulika na uhakiki wa utambulisho wa washiriki wa mikutano ya Shirika la Utalii la Umoja wa Mataifa (UN-TOURISM).

Uchaguzi huo umefanyika katika Mkutano wa 68 wa Shirika hilo kwa Kanda ya Afrika, unaoendelea jijini Abuja, nchini Nigeria.

Mojawapo ya majukumu makuu ya kamati hiyo ni kukagua na kuthibitisha uhalali wa hati za utambulisho za wajumbe wanaowakilisha nchi wanachama, wanachama washirika pamoja na waangalizi wanaoshiriki mikutano ya shirika hilo.

Katika mkutano huo, ujumbe wa Tanzania unaongozwa na Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mhe. Dunstan Kitandula, ambaye anamwakilisha Waziri wa Maliasili na Utalii, Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana.



Akihitimisha siku ya kwanza ya mkutano huo, Katibu Mkuu wa Shirika la Utalii la Umoja wa Mataifa, Zurab Pololikashvili, ameeleza kuwa Afrika ni mojawapo ya maeneo yanayowavutia sana watalii duniani kutokana na mandhari yake ya asili ambayo hayajaharibiwa au kubadilishwa sana.




Kuteuliwa kwa Tanzania katika nafasi hiyo ni ushahidi tosha kuwa nchi kupiga hatua kubwa katika sekta ya utalii barani Afrika.

Ikumbukwe kuwa mwezi Machi mwaka huu, Tanzania ilikuwa mwenyeji wa Kongamano Kubwa la Vyakula Asilia Duniani lililoandaliwa na Shirika la Utalii la Umoja wa Mataifa, ambapo washiriki kutoka kila pembe ya dunia walihudhuria kongamano hilo lililofanyika jijini Arusha.



# SERIKALI KUJENGA UKUMBI MKUBWA WA KIMATAIFA WA MIKUTANO ARUSHA

**Na Mwandishi Wetu**

Katika juhudi za kuimarisha Utalii wa Mikutano na Matukio (MICE) nchini, Serikali kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii imeanza mchakato wa ujenzi wa Ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano (Convention Centre) katika Mkoa wa Arusha, ambao utakuwa na uwezo wa kuchukua washiriki zaidi ya 6,000 kwa wakati mmoja.

Taarifa hiyo imetolewa leo, Juni 6, 2025, na Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mhe. Dastan Kitandula, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana, katika ufunguzi wa Maonyesho ya Karibu-Kilifair 2025 yanayofanyika katika viwanja vya Magereza, Kisongo, jijini Arusha.

Mhe. Kitandula amesema kuwa kwa sasa Utalii wa Mikutano na Matukio unaendelea kukua kwa kasi, hasa katika Mkoa wa Arusha, na hivyo Serikali imeona umuhimu wa kuwekeza katika miundombinu ya kisasa ili kuboresha zaidi mazingira ya kuvutia mikutano na matukio ya kimataifa.

"Serikali imeshatangaza zabuni ya ujenzi wa Ukumbi huu mkubwa wa Kimataifa, ambao unatekelezwa chini ya usimamizi wa Taasisi ya AICC," amesema Mhe. Kitandula.

Ameongeza kuwa mradi huo pia utajumuisha hoteli za kisasa zenye uwezo wa kuwahudumia Marais watano kwa wakati mmoja, pamoja na kuwepo kwa huduma zote muhimu za kimataifa, ili kuhakikisha mazingira bora na ya kuvutia kwa washiriki wa mikutano na maonesho kutoka ndani na nje ya nchi.





# WAZIRI CHANA AIPONGEZA FAMILIA YA CHIFU MKWAWA

**Na Mwandishi Wetu**

Waziri wa Maliasili na Utalii Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana (Mb) ameipongeza familia ya Chifu wa Kabila la Wahehe Adam Abdul Sapi Mkwawa II kwa kuendelea kushirikiana vyema na Serikali katika uhifadhi endelevu wa historia adhimu ya Chifu Mkwawa.

Mhe. Chana ameyasema hayo Juni 5, 2025 Jijini Dodoma alipofunga kikao baina ya wataalam wa Wizara hiyo na Familia ya Chifu Mkwawa kilicholenga kujadili uhifadhi endelevu wa eneo la Kalenga ambalo ni ngome ya aliekuwa Chifu wa kabila la Wahehe, Mkoani Iringa.

Aidha, Mhe. Chana ametumia fursa hiyo kutoa wito kwa Mikoa na Wilaya nchini kuvitambua vivutio vya utalii vilivyopo katika maeneo yao na kisha kupendekeza kwa Wizara ya Maliasili na Utalii kwa lengo la kuvitangaza kuwa vivutio vya utalii.

Kikao hicho kimehudhuriwa na Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Maliasili na Utalii (anayeshughulikia Maliasili ), CP Benedict Wakulyamba, Mkurugenzi wa Idara ya Malikale, Dkt. Christowaja Ntandu na baadhi ya Maafisa Waandamizi kutoka Wizarani na TANAPA.





# TANZANIA NA EU KUSHIRIKIANA SEKTA YA MALIASILI NA UTALII

**Na Mwandishi Wetu**

Waziri wa Maliasili na Utalii Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana amekutana na ujumbe kutoka Umoja wa Ulaya (EU) ukiongozwa na Balozi wa Umoja wa Ulaya nchini Tanzania, Mhe, Christine Grau kwenye Ofisi za Wizara ya Maliasili na Utalii, jijini Dodoma Juni 4,2025.

Katika kikao hicho wamejadiliana ushirikiano katika Sekta ya Maliasili na Utalii hususan katika uhifadhi wa mazingira, uchumi wa bluu, ufugaji nyuki na uzuiaji wa uwindaji haramu wa mazao ya misitu na wanyamapori.

Akizungumza katika kikao hicho Mhe. Chana ameomba Umoja wa Ulaya kusaidia uwekezaji wa kiteknolojia na utafiti katika nishati safi ya kupikia, viwanda vya Misitu na kusaidia uanzishwaji wa Maabara ya Sanaa ya Misitu katika Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania – TAFORI.

Aidha, Mhe. Chana ameiomba EU kusaidia katika Utekelezaji wa Programu mpya ya Maendeleo ya ufugaji nyuki inayozingatia uboreshaji wa maisha hasa kwa jamii katika utoaji wa ajira hasa kwa vijana na wanawake, kusaidia uhifadhi wa rasilimali za nyuki na maliasili nyinginezo ,kuongeza uzalishaji wa mazao ya nyuki na kuuza hasa kwenye soko la kimataifa na kuanzisha awamu ya pili ya mradi wa BEVAC.



Kuhusu matumizi ya Nishati Safi ya kupikia Mhe. Chana amefafanua kuwa zaidi ya asilimia 90% ya kaya nchini Tanzania zinategemea mkaa na kuni kwa ajili ya kupikia jambo linalochangia takriban asilimia 54 ya ukataji miti hivyo kwa kuwekeza katika nishati safi, kutaepusha ukataji miti hovyo na utunzaji wa ardhi kwa maendeleo ya Taifa.

Naye, Balozi wa Umoja wa Ulaya nchini Tanzania, Mhe, Christine Grau amesema Umoja wa Ulaya uko tayari kutoa ushirikiano wa kutosha katika kuiendeleza Sekta ya Maliasili na Utalii.

Amesema pia EU imeanzisha programu ya nishati safi ya kupikia, kusaidia kituo cha taifa cha biashara ya kaboni, kuzuia biashara haramu ya mazao ya misitu na wanyamapori.





# WAZIRI CHANA AWAPONGEZA TAWA KWA KUBUNI MKAKATI WA UWEKEZAJI ZANZIBAR

**Na Mwandishi Wetu**

Waziri wa Maliasili na Utalii Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana amepongeza Bodi ya Wakurugenzi inayoongozwa na Mej.Jen (Mstaafu) Hamis Semfuko pamoja na Menegimenti ya Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA) kwa kubuni mikakati ya uwekezaji katika Bustani ya Wanyamapori Zanzibar.

Mhe. Chana ametoa pongezi hizo wakati akipitishwa katika wasilisho kuhusu fursa za uwekezaji wa Bustani ya Wanyamapori Zanzibar inayotarajiwa kufanyika katika Hifadhi ya Jambiani Muyuni katika kikao kilichofanyika kwenye ukumbi wa Hotel ya Serena, Zanzibar June 25,2025

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya TAWA, Mej. Jen (Mstaafu) Hamis Semfuko amesema uwekezaji wa Bustani ya Wanyamapori katika Hifadhi ya Jambiani Muyuni unatarajiwa kuwa wa viwango vya juu na ukamilikaji wake utaenda kuongeza idadi ya watalii visiwani Zanzibar na Tanzania kwa ujumla sambamba na kuongeza fursa za ajira kwa wananchi wa Zanzibar na Tanzania Bara.



# BOT: WATALII WATAENDELEA KULIPIA KWA FEDHA ZA KIGENI



**Na Mwandishi Wetu**

Benki Kuu ya Tanzania (BoT) imesema Kanuni za Matumizi ya Fedha za Kigeni za Mwaka 2025, inaekeleza malipo ya bidhaa na huduma kati ya wakazi na wageni, wakiwemo watalii yanaweza kufanyika kwa kutumia fedha za kigeni.

Hayo yamesemwa na Mkurugenzi wa Masoko ya Fedha wa BoT, Emmanuel Akaro hivi karibuni jijini Arusha kwenye maonesho ya Karibu-Kilifair.

Akaro amesema hatua hiyo inalenga kuwezesha mazingira rafiki ya kibiashara kwa wageni na urahisi wa miamala katika sekta ya utalii.

"Mawakala wa utalii ambao ni wakaazi, wanaruhusiwa kutumia fedha za kigeni kulipia huduma mbalimbali zinazotolewa kwa watalii kutoka nje ya nchi," amesema Akaro.

Mkurugenzi huyo amesema malipo yote kati ya wakaazi lazima yafanyike kwa Shilingi ya Tanzania na ni kosa kwa mtoa huduma yeyote kukataa malipo yanayofanyika kwa kutumia Shilingi ya Tanzania.



Akaro amesema kanuni hizo zimetungwa kwa mujibu wa Kifungu cha 26 cha Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania ya mwaka 2006, na zimeanza kutumika rasmi kuanzia tarehe 28 Machi 2025.

“Tangu kuanza kutumika kwa kanuni hizo, kumekuwa na matokeo chanya ikiwemo kuongezeka kwa ukwasi wa fedha za kigeni.

Kwa mfano, miamala ya Dola za Marekani kwenye soko la fedha za kigeni la rejareja nchini imeongezeka kutoka wastani wa dola milioni 40 hadi milioni 69 kwa siku,” amesema.




Vilevile, amebainisha kutokana na kuongezeka kwa ukwasi wa fedha za kigeni, thamani ya Shilingi ya Tanzania dhidi ya Dola ya Marekani imeimarika kwa kiwango kikubwa na matarajio ni kwamba itaendelea kuimarika zaidi.

“Hii ni kutokana na kuanza kwa msimu wa mapato ya fedha za kigeni, hususan kutoka kwenye sekta kama utalii, kilimo na mauzo ya bidhaa nje ya nchi, ambazo kwa kawaida huingiza fedha nyingi za kigeni katika kipindi hiki,” amesema.



# BODI YA TATU YA WADHAMINI YA TaFF YAPONGEZWA KWA UTENDAJI ULIOTUKUKA

## Na Mwandishi Wetu

Waziri wa Maliasili na Utalii, Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana (Mb) ameipongeza Bodi ya Tatu ya Wadhamini ya Mfuko wa Misitu Tanzania (TaFF) kwa utendaji kazi uliotukuka katika kipindi cha miaka 3 ya Utekelezaji wa Majukumu katika kusimamia mfuko huo.

Ameyasema hayo Juni 23, 2025 katika hafla fupi ya kuagana na Bodi ya Tatu ya Wadhamini ya Mfuko wa TaFF iliyofanyika katika ukumbi wa Chuo cha Taifa cha Utalii (NCT) jijini Dar es Salaam.

“Kwa kweli mmefanya kazi iliyotukuka kwa kuwa kwa kipindi chote cha miaka mitatu ya utendaji wenu, Wizara haijapokea malalamiko ya migongano ya kimaslahi, migongano kati ya Bodi na Wizara, migongano kati ya Bodi na Menejimenti ya TaFF na migongano kati ya Mwenyekiti na Wajumbe.

Hali imeiifanya TaFF kutekeleza majukumu yake kwa ufasha na ufanisi mkubwa hadi kutambuliwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama Mfuko wa mfano ndani ya Wizara ya Maliasili na Utalii.” Amesema Mhe. Chana.



Mhe. Chana amefafanua kuwa katika kipindi miaka mitatu ya utendaji wa Bodi hiyo, miradi ya kuboresha uhifadhi, uendelezaji na usimamizi wa rasilimali misitu iliyopatiwa ruzuku na Mfuko wa Misitu Tanzania iliongezeka kutoka 738 mwaka 2021/2022 hadi kufikia miradi 1,196 mwaka 2024/2025.

Naye, Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini ya Mfuko wa Misitu Tanzania, Prof. Shabani Chamshama amesema katika kipindi cha miaka mitatu ya bodi hiyo imefanikiwa kuendelea kutoa ruzuku na kuwezesha ongezeko la miradi iliyopatiwa ruzuku na fedha za tozo ya upandaji miti kutoka miradi 738 mwaka2021/2022 hadi kufikia miradi 1,196 mwaka 2024/2025 ambayo imechangia kuboresha uhifadhi, usimamizi na uendelezaji wa rasilimali misitu nchini na upatikanaji wa ajira.

Kikao hicho kimehudhuriwa na Mkurugenzi wa Idara ya Misitu na Nyuki Bw. Deusdedith Bwoyo, Mkurugenzi wa Idara ya Usimamizi wa Rasilimaliwatu, Bernard Marcelline pamoja na baadhi ya Wakurugenzi Wasaidizi na Maafisa Waandamizi kutoka Wizara ya Maliasili na Utalii na TaFF.



# USIYOYAJUA KUHUSU CHIFU ALIYEZIKWA KATIKA KABURI LA MVIRINGO AKIWA AMEKETI MBINGA

## Na Mwandishi Wetu

Katika kijiji cha Mbuji kilichojificha kwenye vilima vya wilaya ya Mbinga mkoani Ruvuma, kuna kaburi la aina yake kaburi linalobeba historia ya maumivu, ujasiri, usaliti, na ushindi.

Hili si kaburi la kawaida, ni kaburi la Jemedari wa vita, Mtawala wa kwanza wa kabila la Wamatengo, Chifu Kayuni Kapitangana Ndunguru Makita, ambaye si tu alipigana vita vya ukombozi dhidi ya Wangoni, bali pia aliuawa kikatili na kisha kuzikwa akiwa amekalishwa katika kaburi la mviringo kama ishara ya heshima kuu kwa mashujaa waliotangulia.

Hii ni hadithi ambayo haijasimuliwa sana, lakini inayobeba uzito mkubwa wa historia ya makabila ya Kusini mwa Tanzania hadithi ya kiongozi aliyekuwa zaidi ya mtawala; alikuwa ngao ya taifa lake.











## MASTAA WAMIMINIKA TANZANIA

Nyota wa Barcelona na timu ya Taifa ya Hispania, Pablo Gavi amefuata nyayo za baadhi ya mastaa wa soka wa nchi yake kwa kuja mapumzikoni Tanzania.

Kiungo huyo alifika katika Hifadhi ya Taifa ya Serengeti sambamba na mpenzi wake, Ana Pelayo.





iamzlatanibrahimovic








pedri 6h
Follow
PILATUS
AURIC
AIR


maihelmy.official
Tyla · Water
6/13
70.1K
312
2,918
maihelmy.official only Me & turtles 🐢 on the island cave 😁... more


41.9K
949
149
Liked by gilbertmayani95 and others
t.trouboul First day of the honeymoon completed 🦒 🐘


theozidane
TANZANIA
139
Liked by tanzania_unforgettable and others
theozidane TZ

**tanzania_unforgettable** and **lother_jose**
AI info



490 10 4

Liked by **tanzania_unforgettable** and **others**
**lother_jose** It was great Having you out here
David Raya. Arsenal Goalkeeper

June 27

# HOTUBA YA BAJETI KUU YA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/26

## MAFANIKIO SEKTA YA MALIASILI NA UTALII

1. Kutokana na kuanzishwa kwa programu maalum za kuitangaza Tanzania kimataifa kama vile filamu ya Tanzania – The Royal Tour pamoja na filamu ya Amazing Tanzania idadi ya watalii imeongezeka kutoka watalii 1,183,416 mwaka 2020 hadi watalii 5,360,247 mwaka 2024.

2. Mapato yatokanayo na watalii wa nje ya nchi yameongezeka kutoka dola za Marekani milioni 715.0 mwaka 2020 hadi dola za Marekani bilioni 3.9 mwaka 2024.

3. Mafanikio haya yameiwezesha Tanzania kutambulika kimataifa ambapo imeshika nafasi ya tisa (9) duniani na 53 nafasi ya tatu (3) barani Afrika mwaka 2024 kwa ongezeko la mapato yatokanayo na shughuli za utalii.


4. Tanzania imetambulika kuwa eneo linalovutia zaidi kiutalii barani Afrika (Africa's Leading Destination) kwa mwaka 2024 .

5. Hifadhi ya Taifa ya Serengeti imeendelea kuwa mshindi wa tuzo ya hifadhi bora duniani kwa mara ya tano (5) mfululizo kutoka mwaka 2019 hadi mwaka 2024.



TANZANIA Unforgettable!

wizarayamaliasilinautalii


WORLD TRAVEL AWARDS
WINNER
2025
TANZANIA WINS
1. Africa's Leading Destination 2025-TANZANIA
2. Africa's Leading Elephant Paradise National Park-TARANGIRE
3. Africa's Leading Cultural National Park-RUAHA
4. Africa's Leading honeymoon Destination-KITULO
5. Africa's Leading BIG fIVE national park-SERENGETI
6. Africa's Leading Tourist Board-TANZANIA TOURIST BOARD
7. Africa's Leading Tourist Attraction-NGORONGORO
8. Africa's Leading Scenic National Park-NYERERE
9. Africa's Leading Mountain National Park-KILIMANJARO
10. Africa's Leading National Park-SERENGETI
#TanzaniaShines2025
WORLD TRAVEL AWARDS
TANZANIA
Unforgettable!
wizarayamaliasilinautalii